

BARAZA LA HABARI TANZANIA



S.L.P 10160, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2775728 / 2771947
Simu ya mkononi: +255 719 494640
+255 767 494826 / 784 314880
Nukushi: +255 22 2700370
Barua pepe: media@mct.or.tz
Tovuti: <http://www.mct.or.tz>
S.L.P 3490, Zanzibar
Simu: +255 24 2239728,

P.O. Box 10160, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 22 2775728 / 2771947
Mob: +255 719 494640 / 686 494640
+255 767 494826 / 784 314880
Fax: +255 22 2700370
E-mail: media@mct.or.tz
Website: <http://www.mct.or.tz>
P.O. Box 3490, Zanzibar
Tel: +255 24 2239728

Tamko la Wadau wa Habari Kuhusu Azma ya Serikali Kupeleka Miswada ya Haki ya Kupata Habari na Huduma za Vyombo vya Habari kwa Utaratibu wa Hati ya Dharura

Sisi wadau wa masuala ya habari na upatikanaji wa taarifa tumepokea taarifa za utayari wa miswada muhimu miwili ya Haki ya Kupata Habari (Access to Information Bill) na Huduma za Vyombo vya Habari (Media Services Bill) kwa faraja. Miswada hii imekuwa ikisubiriwa kwa muda mrefu tangu wadau na wananchi walipoanza kuidai ili kusaidia upatikanaji wa taarifa na habari kwa ajili ya maendeleo ya taifa lote kwa ujumla pamoja na kuboresha uendeshaji wa vyombo vya habari.

Tangu muswada ulipotolewa na serikali kwa mara ya kwanza mwezi Oktoba mwaka 2006 na kuondolewa, wadau na wananchi wamekuwa wakitazamia kuwa miswada miwili iliyoboreshwa kutokana na maoni na mapendekezo yao ingewasilishwa bungeni mapema zaidi.

Maoni na mapendekezo ya wadau wa habari juu ya muswada wa Haki ya Kupata Habari wa mwaka 2006 yalikalika na kuwasilishwa serikalini mwaka 2007, na mapendekezo ya muswada wa Huduma za Vyombo vya Habari mwaka 2008. Ni faraja kwa wadau kwamba serikali imeona mantiki ya kuandaa miswada miwili tofauti ya Haki ya Kupata Habari na Huduma za Vyombo vya Habari.

Ni wazi kuwa, kuwasilishwa kwa miswada hii kunaendana na dhamira iliyooneshwa na serikali katika mipango na ahadi zake mbalimbali katika uendeshaji wa shughuli za serikali kwa uwazi. Aidha, miswada hii inaendana na dira ya kuimarisha demokrasia, uwajibikaji na utawala bora pamoja na ushirikishwaji wa wananchi na kuheshimu haki za binaadamu.

Kwa maoni yetu, kukamilika kwa miswada hii, kunatimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais Dk. Jakaya Mrisho Kikwete na serikali kwamba sheria hizo zingetungwa kabla ya kumalizika kwa serikali ya awamu ya nne ya utawala wa nchi yetu. Kutungwa kwa sheria za Haki ya Kupata Habari ni moja ya dhamira za mipango ya kuendesha

